AfCHPR
Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

MUHTASARI WA HUKUMU

M'BA JEAN ROGER

DHIDI YA

BURKINA FASO

MAOMBI NA. 015/2019

HUKUMU KUHUSU
MAMLAKA YA KISHERIA NA UKUBALIFU

TAREHE 13 NOVEMBA 2026

UAMUZI WA MAHAKAMA YA AFRIKA YA HAKI ZA BINADAMU NA WATU

Arusha, tarehe 13 Novemba 2026: Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (Mahakama) imetoa hukumu katika kesi ya *Jean Roger M'BA dhidi ya Burkina Faso.*

Tarehe 23 Aprili 2019, Jean Roger M'BA (Mleta Maombi) aliwasilisha Maombi kwenye Mahakama dhidi ya Burkina Faso (Mjibu Maombi) akidai ukiukaji wa haki zake kuhusiana na kesi zilizosikilizwa katika mahakama za Burkina Faso.

Kuhusu fidia, Mleta Maombi aliiomba Mahakama imwamuru Mjibu Maombi ampe msamaha wa rais; abadilishe hukumu yake ya kifo na hukumu za watu wengine wote waliohukumiwa adhabu hiyo kuwa kifungo cha gerezani; impe msamaha wa masharti; ipange kumsafirisha kwenda katika nchi yake alipozaliwa; msamaha wa jumla; suluhu ya nje ya mahakama; na fidia ya kifedha kutokana na madhara aliyoyapata kwa sababu ya maamuzi 'yasiyo ya haki' ya mahakama yaliyotolewa dhidi yake.

Kwa upande wake, Mjibu Maombi hakuwasilisha maombi yoyote.

Baada ya kubaini kwamba matakwa ya Kanuni ya 63(1) ya Kanuni za Mahakama yalitimizwa, Mahakama iliamua kutoa hukumu moja kwa moja.

Hakuna pingamizi lililowasilishwa dhidi ya mamlaka ya Mahakama kwa kuwa Mjibu Maombi hakujitokeza. Licha ya kutojitokeza kwa Mjibu Maombi, Mahakama iliridhika kwamba matakwa yote yalitimizwa kuhusiana na vipengele vya mamlaka halisi, binafsi, ya muda na ya kieneo na kwa hivyo ilitangaza kwamba ina mamlaka ya kisheria ya kusikiliza Maombi hayo.

Hakuna pingamizi lililowasilishwa dhidi ya ukubalifu wa Maombi kwa kuwa Mjibu Maombi hakujitokeza. Hata hivyo, Mahakama iliridhika kwamba matakwa yote ya ukubalifu yalikuwa yametimizwa. Kwa kuzingatia kwa umahususi takwa la kuwasilisha maombi ndani ya muda unaofaa, Mahakama ilirejea kwamba inazingatia mambo fulani, hasa iwapo mleta maombi anajua kusoma na kuandika au la, iwapo alisaidiwa na wakili na iwapo alikuwa amefungwa gerezani kiasi kwamba hakuweza kutoka kwenda sehemu nyingine na ufikiaji wake wa taarifa ulikuwa mdogo. Mahakama pia ilisisitiza kwamba ni jukumu la mleta maombi kuthibitisha kwamba muda aliotumia kuwasilisha maombi yake ulikuwa unafaa na ikafafanua kwamba ukweli wa kufungwa gerezani haujumuishi sababu ya kuchelewa katika suala hili.

Mahakama ilibaini kwamba Mleta Maombi hakutoa sababu kwa nini ilimchukua miaka sita, miezi miwili na siku 29 baada ya taratibu za ndani kukamilika kuwasilisha Maombi haya. Mahakama pia ilisisitiza kwamba hakukuwa na chochote katika kumbukumbu kinachoonyesha kwamba hajui kusoma na kuandika, ni maskini au hajui kuwa Mahakama hii ipo. Kwa hivyo, iliamua kwamba kipindi kilichotajwa hapo juu hakikuwa kinachofaa kwa kurejelea hukumu zake za awali.

Baada ya kubaini kwamba Maombi haya hayakukidhi takwa la Kanuni ya 50(2)(f) ya Kanuni za Mahakama na kwa kuzingatia kwamba matakwa ya ukubalifu ni ya jumla,

Arusha, Tanzania
Barua pepe: registrar@african-court.org
Wavuti: www.african-court.org
Simu : +255-272-510-510

Mahakama iliamua kwamba hakukuwa na haja ya kutoa uamuzi kuhusu uzingatiaji wa matakwa mengine ya ukubalifu. Kwa hivyo, Mahakama ilitangaza kwamba Maombi hayo hayakubaliki kwa sababu hayakuwasilishwa ndani ya muda unaofaa.

Mahakama iliamua kwamba kila upande unapaswa kubeba gharama zake.

Maelezo zaidi

Taarifa zaidi kuhusu kesi hii, ikiwa ni pamoja na maelezo kamili ya hukumu ya Mahakama ya Afrika, inapatikana kwenye tovuti https://ajudata.african-court.org/fr/details-case/0152019.

Kwa maswali mengine yote, tafadhali wasiliana na Msajili kwa barua pepe registrar@african-court.org.

Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ni mahakama ya bara zima iliyoanzishwa na nchi za Afrika ili kuhakikisha ulinzi wa haki za binadamu na watu barani Afrika. Mamlaka ya Kisheria ya Mahakama kusikiliza kesi na mizozo yote iliyowasilishwa kwake kuhusu tafsiri na utekelezaji wa Mkataba wa Afrika kuhusu Haki za Binadamu na Watu na chombo kingine chochote cha Haki za Binadamu kilichoidhinishwa na Nchi zinazohusika. Kwa maelezo zaidi, tafadhali tembelea tovuti yetu www.african-court.org.